

Ubeberu wa Wareno na Kaburu wajadiliwa UNO

BARAZA la Usalama UNO limekutana jana kujadilia rai iliyotolewa na nchi thelathini na mbili za Kiafrika juu ya Afrika Kusini na hali ilivyo katika makoloni ya Kireno hapa Afrika.

Nchi hizi 32 za Kiafrika zilieleza katika barua mbali mbali zilizotangazwa mjini New York Julai 12 mwaka huu kuwa siasa ya Afrika Kusini na hali iliyoko katika makoloni ya Wareno hapa Afrika ni kitisho kikubwa kwa amani ya ulimwengu. Nchi hizo za Kiafrika zikaomba, "Baraza la Usalama la UNO lichukue hatua mapema kuma iwezekanavyo."

Kuhusu Swali la ubaguzi, nchi zile za Kiafrika zikaomba Baraza la Usalama kuchukua hatua ya kufaa kutafuta iawabu linalolingana na maazimio ya Baraza Kuu la UNO.

Tatizo kubwa

Habari zilizofika hapa zinasema kuwa mwende ndo huu umetokana moja kwa moja na maazimio yaliyopitishwa na vichwa wa nchi za Kiafrika kwenye mkutano wa Addis

wa mkutano wa maana sana katika historia ya Afrika; na kila barua ya zile nchi 32 ikafuatwa na kumbukumbu kueleza uvundo wa siasa ya Ubaguzi.

Wale waliotia sahihi zao katika kumbu kumbu hizi wanasema jambo la ubaguzi ni tatizo kubwa sana kwa nchi za Kiafrika.

Ababa katika mwezi Mei. Kila moja ya barua zile iliutaja mkutano ule wa vichwa vya nchi huru za Kiafrika kuwa uliku-